# HIGH AIMERS SERIES
# DARASA LA NANE - 2022

Muda: Saa 1 Dak. 40

# KISWAHILI : LUGHA

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandik[illegible] majibu.

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba ako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za [illegible] katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1- 50 umepewa majibu manne. Majibu [illegible] yameonyeshwa kwa herufi A, B,D na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hili.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa [illegible] katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**
**Katika kijitabu cha maswali:**

21. Nafasi iliyotengenezwa ukutani ili kuwekea vitu ni:-
    A. sefu
    B. shubaka
    C. rafu
    D. kabati

Jibu sahihi ni **B** (shubaka)
Katika karatasi ya majibu

**20.** [A] [B] [C] [D] **21.** [A] [~~B~~] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **23.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku ulivyopewa.

**Kitabu jhiki cha maswali kila kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**SKY FLYER EDUCATIONAL PUBLISHERS**
*Email:- skyflyerexams@gmail.com*

**Geuza ukurasa**

***Soma vifungu vifuatavyo vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

Mechi __1__ imepamba moto. Kila mchezaji __2__ ili kusaidia timu __3__ kufunga bao. Refa alionekana akihema uwanjani kwa sababu ya kukimbia huku na __4__ kwa sababu pasi __5__ safi na za haraka __6__ nao walifurahisha macho hata wakasahau kushangilia na kuwahimiza wachezaji wa timu zao. Tofauti na kawaida, siku hiyo uwanja __7__ umetulia hata bila kelele za walioshabikia. Kila shabiki alikuwa na __8__. Mabao yalikuwa mawili kwa mawili. Muda ulikuwa __9__ dakika kumi tu ili mechi ikamilike. Kilikuwa kipindi cha lala salama.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. zilikuwa | B. itakuwa | C. ulikuwa | D. ilikuwa |
| 2. | A. walijizatiti | B. alizembea | C. alijizatiti | D. atajizatiti |
| 3. | A. lao | B. zake | C. yake | D. zote |
| 4. | A. huko | B. pale | C. kule | D. hapa |
| 5. | A. ilikuwa | B. zilikuwa | C. zitakuwa | D. yalikuwa |
| 6. | A. Washabiki | B. Mashabiki | C. Shabiki | D. Wachezaji |
| 7. | A. alikuwa | B. utakuwa | C. zilikuwa | D. ulikuwa |
| 8. | A. roho mkononi | B. wasiwasi mwingi | C. moyo mkononi | D. kichwa kizito |
| 9. | A. umesalia | B. imebaki | C. umekamilisha | D. umeisha |

Jikoni ni mahali ambapo __10__ huandaliwa. Shughuli hii ya kuandaa chakula haiwezi kukamilika bila usaidizi wa vifaa __11__. Jokofu ambalo pia huitwa __12__ husaidia kuhifadhi vyakula ili visiharibike. __13__ ambalo ni jiko la makaa hutumiwa kupikia vyakula hasa vile ambavyo huchukua muda mrefu kuiva. Sinki au __14__ ni mahali pa kuoshea vyombo. Tukitaka kukamata au kushika sufuria tunapopika sisi hutumia __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. maankuli | B. makuli | C. maakuli | D. mankuli |
| 11. | A. kadhaa wa kadhaa | B. kadha | C. kadha wa kadha | D. kadhaa |
| 12. | A. jirafu | B. friji | C. sinia | D. kawa |
| 13. | A. Seredani | B. Stovu | C. Figa | D. Chujio |
| 14. | A. charo | B. beseni | C. karo | D. bilula |
| 15. | A. kamaki | B. boi | C. kamata | D. kibandiko |

**Kutoka Swali la16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo.**

16. Ainisha aina ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi.

<u>Chako</u> kina rangi nzuri <u>lakini</u> vingine havipendezi.

A. Kivumishi kimilikishi, kiwakilishi

B. Kiwakilishi kimilikishi, kiunganifu

C. Kivumishi, kiunganishi

D. Kimilikishi cha nafsi ya pili, kiunganishi

17. **Chagua ukanusho sahihi.**

Gurudumu ambalo limetoboka litauzwa kwa fundi.

A. Gurudumu ambalo limetoboka halitauzwa kwa fundi

B. Gurudumu ambalo halijatoboka halitauzwa kwa fundi

C. Magurudumu ambayo hayajatoboka hayatauzwa kwa mafundi

D. Gurudumu ambalo limetoboka halijauzwa kwa fundi

18. Unda nomino dhahania kutokana na kitenzi **lima**.

A. kilimo

B. kulima

C. mkulima

D. ukulima

19. **Chagua umoja wa udogo wa sentensi hii.**

Mawe makubwa yaliwaangukia nyoka wakafa.

A. Kijiwe kikubwa kilikiangukia kijoka kikafa

B. Vijijiwe vidogo viliviangukia vijoka vikafa

C. Jijiwe kubwa liliangukia joka likafa

D. Kijijiwe kikubwa kulikiangukia kijoka kikafa

20. Chagua maelezo yaliyo sahihi.

A. Dunia ni sayari ya nne na ndiyo kubwa zaidi ya zote

B. Mirihi ndiyo sayari ndogo zaidi na ni ya tatu kutoka kwa jua

C. Zaibaki ndiyo sayari ya kwanza kutoka kwa jua

D. Kuna jumla ya sayari kumi

21. Chagua orodha yenye vibadala.

A. Hasira - furaha

B. Ukuta - kiambaza

C. Chakula - chakura

D. Blanketi - blangeti

22. Mapambo haya yote huvaliwa katika sehemu za kichwa ila;

A. kipini

B. siniguse

C. bali

D. mapete

23. Wanafunzi walianza safari ya kuelekea katika mbuga ya wanyama saa nne asubuhi. Safari ikachukua muda wa saa nne na robo. Je, safari ilitia nanga saa ngapi?

A. Saa nane na robo

B. Saa nne na robo

C. Saa tisa na kasorobo

D. Saa nane na dakika kumi na tano

24. Mfupa ambao hupatikana kwenye mguu baina ya goti na wayo huitwa,

A. tokoni

B. fuvu

C. utaya

D. muundi

25. Chagua orodha inayotiririsha vitendo vya shambani.

A. Kufyeka, kulima, kupanda, kupalilia, kuvuna

B. Kufyeka, kupanda, kulima, kupalilia, kuvuna

C. Kupalilia, kufyeka, kulima, kupanda, kuvuna

D. Kulima, kupalilia, kupanda, kuvuna

26. Ni neno lipi lina aina tatu za silabi?

A. Lalia

B. Ingia

C. Mwagia

D. Rahisi

27. Jana ilikuwa Jumapili tarehe nne. Kesho kutwa itakuwa siku gani na tarehe ipi?

A. Jumatatu tarehe tano

B. Jumatano tarehe sita

C. Jumatano tarehe saba

D. Jumanne tarehe sita

28. Chagua sentensi yenye kielezi cha wakati.

A. Vitabu vyote vimewekwa mezani penye uwazi

B. Wanafunzi wa darasa la nane watafanya mtihani mwakani

C. Watakapofika nyumbani watalakiwa kwa shangwe

D. Walimu wetu hujikaza kisabuni ili kutuongoza ipasavyo

29. Andika sentensi hii katika usemi halisi;

Daktari aliwataka wagonjwa wote wavae maski.

A. "Nilitaka nyinyi nyote mvae maski." daktari aliwaambia wagonjwa.

B. Daktari: Nataka nyinyi wagonjwa nyote mvae maski

C. "Vaeni maski zenu haraka." daktari aliwaamuru wagonjwa.

D. "Je, mnaweza kuvaa maski zenu?" daktari aliwauliza wagonjwa wote

30. Eleza maana ya semi;

Kuenda nguu.

A. Kuchoka sana

B. Kushindwa katika mashindano

C. Kupata nafuu

D. Kupoteza matumaini

***Soma kifungu hiki kisha uyajibu maswali 31 - 40.***

"Mwalimu mkuu bwana Simba Chudi, Naibu wa mwalimu mkuu Bi. Chiriku Mpole, wadarisi na wangenzi wapendwa, sabalkheri? Leo ni siku njema ambayo Mola ametutunukia. Mimi ni Bahati binti Idili, kiranja mkuu hapa shuleni. Nimesimama <u>mkabala</u> wenu ili kueleza kuhusu mbinu za kuzingatia usafi wa mazingira.

Ni muhimu kuyasafisha mazingira. Kwanza kabisa tunaweza kuokota takataka, kuzikusanya na kuzizika au kuzichoma. Takataka huchafua mazingira yetu. Shughuli hii ya kuokota na kuchoma taka inaweza kufanywa nyumbani, shuleni, barabarani, kanisani na hata penye maeneo ya burudani.

Shuleni, tunafaa kuwasaidia wafanyakazi kupangusa madawati na kupiga deki. Mle darasani, hatufai kutupa takataka ovyoovyo pasi kutumia jalala. Hata tunapoandika vitabuni,tunafaa kuutumia mwandiko safi na unaoweza kusomeka kwa urahisi. Hatufai kwaga mwaga wino kitabuni au dawatini. Vitabu vyetu pia vinafaa kuwa na jalada kila wakati. Hatufai kurarua kurasa zozote zile.

Fauka ya hayo, tunaweza kushirikiana na walimu na wafanyakazi wengine ili kupuliza dawa ya kuangamiza <u>vimelea</u> kama vile kunguni na chawa. Vitanda tunavyovilalia shuleni na hata nyumbani vinaweza kuwekwa safi kwa kuua vimelea hawa. Nyasi ndefu zinafaa kufyekwa ili kuwafukuza mbu ambao husambaza maradhi ya malaria. Tukifanya hivyo, tutakomesha maambukizi ya maradhi mengi yakiwemo malaria na kichocho.

Shambani panafaa kuwa safi vilevile. Je, tunawezaje kuhakikisha kuwa kule shambani ni safi? Ninajua mnashangaa sana. Lakini, tunapoondoa magugu shambani na kubaki na mimea tu, huwa tumesafisha shamba. Shamba likishakuwa safi bila magugu, basi mazao huwa mazuri na chungu nzima.

Mavazi yetu yanafaa kuoshwa kwa maji safi na sabuni. Baada ya kukauka, ni vyema pia yapigwe pasi kwa yale ambayo yanaweza kupigwa pasi. Nguo safi hunukia vizuri na pia huwafukuza vimelea. Mili pia ni miongoni mwa vitu vilivyounda mazingira. Mili isipokuwa safi, **<u>hunuka fee!</u>** Mili safi hupendeza. Hatimaye, yote yatakuwa ,mambo ya bure iwapo tutakosa kuzingatia usafi wa akili na mawazo. Kila mmoja wetu anafaa kuzingatia fikra safi na matendo mema. Mwanafunzi mwenye akili safi, huwa na tabia ya kupendeza. Bila shaka, ni dhahiri kuwa usafi una mbinu nyingij za kuudumisha. Nasi hatuna budi ila kuwajibika."

**31.** Chagua kikundi ambacho hakikuwa miongoni mwa hadhira ya hotuba hii.

A. Wabyele

B. Wanafunzi

C. Walimu

D. Naibu wa mwalimu mkuu

**32.** Neno mkabala limepigiwa mstari. Je, maana yake ni gani?

A. Kusimama karibu na kitu

B. Kusimama kando kando ya kitu

C. Kusimama na kuangalia uso kwa uso na kitu

D. Kusimama nyuma ya kitu

**33.** Aya ya tano imebainisha kuwa;

A. magugu hufanya shamba lionekane chafu hata kama mazao huwa mengi

B. mimea ikiwa mingi shambani, magugu hayawezi kupatikana

C. kwekwe zikitolewa shambani, mazao yatakuwa tele na mema

D. usafi wa shambani hutegemea sana maji

**34.** Toa maelezo ya usemi kupiga deki kaa ulivyotumika katika ufahamu.

A. Kupanda juu ya kitu chenye ghorofa

B. Kupangusa sakafu kwa kutumia kitambaa na maji

C. Kupangusa vifaa kama meza na viti

D. Kupiga akili ili kufahamu jambo zuri la kutenda

**35.** Taja hatibu wa hotuba hii.

A. Mwanafunzi ambaye ndiye mwakilishi wa wanafunzi wengine wote

B. Mwalimu mwakilishi wa wanafunzi wote

C. Mwanafunzi ambaye ndiye kiongozi wa wanafunzi wengine wote

D. Mwalimu aliyewakilisha wanafunzi na walimu wengine wote

**36.** Shughuli hii ya hotuba ilifanyika wakati gani wa siku?

A. Wakati wa asubuhi

B. Wakati wa jioni

C. Wakati wa usiku kabla ya watu kulala

D. Wakati wa adhuhuri walipokuwa wakila chamcha

**37.** Kifungu kimedhihirisha kwamba;

A. tukiosha na kuzipiga nguo pasi, huwa tunawazuia vimelea

B. Usafi wa akili na fikra ni wa mwisho na hivyo basi hauna maana sawa

C. kunguni na chawa ndio vimelea pekee wanaopenda usafi

D. takataka huongeza mbolea kwa ardhi kwa hivyo hazifai kuondolewa

**38.** Madai haya yote ni ya kweli kwa mujibu wa aya ya tatu isipokuwa moja. Itaje.

A. Mwandiko mwema na safi husaidia kusafisha mazingira

B. Matumizi ya jalala darasani ni muhimu katika harakati za kusafisha mazingira

C. Wino ukimwagwa na kutapakaa vitabuni, huwa ni uchafuzi wa mazingira

D. Walimu huwa kielelezo kwa wanafunzi hasa jinsi wanapovaa mavazi safi

**39.** Katika aya ya nne, neno vimelea limepigiwa mstari. Gani kati ya hawa si kimelea?

A. Mbu

B. Mende

C. Chawa

D. Kunguni

**40.** Kichwa kifaacho makala haya ni;

A. Madhara ya usafi wa mazingira

B. Njia za kuangazia usafi wa mazingira

C. Mazingira na faida zake

D. Mazingira yetu

*Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.*

Mamba ni wanyama ambao husonga kwa kutambaa na ni wakubwa. Hupatikana katika maeneo ya joto zaidi duniani. Familia ya mamba ina aina ishirini na tatu. Mamba kwa namna fulani wamekuwa duniani kwa karibu miaka milioni sitini na mitano.

Mamba wa Kiafrika huwa na urefu wa futi sita, naye mamba wa maji ya chumvi, hukua hadi zaidi ya futi ishirini kwa urefu. Mamba wana mili mikubwa na mipana, miguu minne mifupi na mkia mrefu wenye misuli. Wana ngozi nene yenye magamba magumu. Meno yao yana umbo la pia na yamejitokeza kando kando ya utaya. Mnyama huyu huendelea kukua na kuongeza urefu na uzito. Ana uwezo wa kuishi hadi miaka sabini na mitano.

Wanyama huwa wanaweza kukaa ardhini na pia majini. Wanapenda sana kukaa majini wakisubiri kuwinda. Aghalabu wao huja tu ardhini ili kuota jua. Mamba hupatikana kote duniani lakini wengi hupatikana katika maeneo yenye joto zaidi kama Amerika na Afrika. Mili yao mikubwa ni mizito wakiwa kwenye ardhi lakini ni wepesi zaidi ndani ya maji. Huogelea kwa mwendo wa kasi sana.

Wanyama hawa hula nyama tu. Hawali majani. Wana uwezo wa kuvunjavunja hata mifupa. Tumbo lao lina asidi ambayo husaidia kusaga chakula hata ngozi na mifupa. Mamba hunyemelea windo lake na kuvamia ghafla. Mkia wake humsaidia sana kuzamisha windo lake kwa upesi sana. Baada ya windo kufa, mamba huja kwa wingi na kulirarua raruraru. Wao huwa hawatafuni nyama ila huimeza tu. Wakishashiba, hutoka majini na kujianika ufuoni ili kuota jua.

Mamba huwa ni wanyama wasiri sana. Akiwa majini huwa hataki kushirikiana na wengine pengine tu katika shughuli ya kuwinda. Umoja wao huonekana vyema wakati wa kuwalea wana. Wote huwa na ushirika wa kipekee hata kama watoto si wao. Wanyama hawa hutaga takribani mayai thelathini kwa wakati mmoja. Mayai haya hutagiwa kandokando ya maji yaani **ufuoni** penye vichaka. Baada ya kuanguliwa, mamba huwabeba watoto wao hadi majini ili kuwanusuru wasiliwe na wanyama wengine kama vile nyoka, paka na hata mbwa mwitu.

41. Taja kisawe cha neno mamba.
    A. Mburukenge
    B. Mjusi
    C. Ngwena
    D. Kasa

42. Jina ufuoni limepigwa mstari. Je, lina maana gani kwa mjibu wa ufahamu?
    A. Katikati ya mto
    B. Mahali ambapo maji yameenda chini zaidi
    C. Mahali penye mchanga ama ardhi kando kando ya mto, ziwa au bahari
    D. Sehemu ya mto ambapo maji huteremka kwa kasi sana

43. Gani si sifa ya mamba kulingana na kifungu?

A. Ana mkia mnene na wenye nguvu

B. Ana meno makubwa na makali ya kutafunia nyama kabla ya kumeza

C. Ana miguu minne na mifupi

D. Anapenda sana kukaa majini hasa kabla hajashiba

44. Ni sababu gani humwezesha mamba kusaga chakula kigumu kama vile mifupa na ngozi?

A. Meno yake makubwa na yenye nguvu sana

B. Ngozi yake ngumu na yenye magamba

C. Kuwepo kwa asidi tumboni mwake

D. Kuwepo kwa asidi mdomoni mwake

45. Ni madai gani ya kweli kwa mujibu wa aya ya tatu?

A. Mamba wanapatikana kila sehemu ya dunia kwa idadi sawa

B. Mamba wengi wanapatikana Amerika na Afrika kwa sababu ya kiwango cha wastani cha joto

C. Mara nyingi mamba wanapopatikana ardhini, huwa ni sababu ya kutafuta joto

D. Afrika na Amerika ni baadhi ya maeneo yenye joto jingi

46. Iwapo mamba atataga mayai mara tano katika maisha yake, basi atakuwa ametaga jumla ya mayai mangapi?

A. Takribani mayai thelathini

B. Mayai thelathini

C. Mayai mia moja hamsini

D. Takribani mayai mia moja hamsini

47. Eleza maana ya neno kutambaa kama ilivyotumika katika ufahamu.

A. Kusonga kwa miguu mingi na kwa haraka

B. Kusonga kwa miguu mifupi iliyokaribia kugusa ardhi

C. Kusonga kwa kuburura makalio kwenye ardhi

D. Usongaji wa wanyama ambao hawana miguu

48. Chagua maelezo yaliyo sahihi kwa mujibu wa ufahamu huu.

A. Mamba huwa hafukuzi windo lake ila huotea na kuvamia bila kutarajiwa

B. Baada ya mayai kuanguliwa, watoto wa mimba hukimbilia majini ili wasiliwe na wanyama wengine

C. Mbwa mwitu na nyoka ni baadhi ya wanyama wanao kula mayai ya mamba

D. Mamba wana uwezo wa kutafuna mifupa

49. Mamba wamekuwa duniani kwa takribani miaka milioni sitini. Hivi ni kusema kwamba;

A. 60000000

B. 6000000

C. 600000000

D. 6000600

50. Ni mada gani mwafaka kwa makala haya?

A. Wanyama wa majini

B. Faida za mamba

C. Maisha ya mamba

D. Mamba na watoto wake